Jiwe la kujengea la kiroho Na. 180

# Kile Kiti Cha Hukumu Cha Kristo

*2 Wakorintho 5:10-11*

*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyoyatenda katika mwili, kadiri alivyotenda kwamba ni mema au mabaya. Basi tukijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu; lakini tumedhihirishwa mbele za Mungu, Nami natumaini ya kuwa tumedhihirishwa katika dhamiri zenu pia.*

Nabii wa Mungu ndugu Branham, alieleza ndoto:

Nataka kuwaambieni jambo dogo lililotokea. Ilikuwa ni ndoto. Nilikuwa nimelala. Na sasa sijalisema hili mbele ya kadamnasi. Nimewaambia baadhi ya watu lakini kamwe sijalizungumzia Miongoni mwa watu wengi kwa kadiri nijuavyo.

Niliota kama mwezi mmoja baadaye kwamba siku moja nilikuwa nimesimama na nilikuwa ninaangalia ule wakati mkuu ambao---- siyo hukumu sasa, siamini kama kanisa litakuja- Na maanisha Bibi Arusi kwamba ataingia hukumuni- lakini nilikuwa pale wakati wakipewa taji (1Korintho 4:5)

Na kile kiti kikuu kiliwekwa pale na nilikuwa nimesimama pale. Yesu na Malaika anayeweka rekodi na wote walikuwa wamesimama pale. Na palikuwa na kitu kama ngazi upigapo hatua kuja upande huu wa kiti cheupe cha pembe (ambayo iko kama duara na ilitengeneza panora kama hivi na ikaendelea) kiasi kwamba umati huu mkubwa ulisimama pale na niliweza kuona kilichokuwa kinatokea.

Na nilikuwa nimesimama mbali upande mmoja. Na nilikuwa nimesimama tu pale, kamwe sina wazo lolote kwamba ningetembea kwenye hiyo ngazi. Nilikuwa nimesimama pale, na nilimuona Malaika awekae rekodi naye angeita Jina fulani, na ninajua—nilitambua hilo jina. Niliangalia na nyuma nje pale, alikuja hapa ndugu akitembea au dada, akitembea juu pale kama hivi. Yule Malaika aneyeweka rekodi amesimama pale upandeni kwa Yesu (ni ndoto tu sasa) na nilikuwa nikiangalia majina yao yalikuwepo, yalionekana kwenye kitabu cha uzima. Angewaangalia nje kule angesema, “Vema mtumwa mwema na mwaminifu” ingai ndani.

Nikiangalia kule walikokuwa wanakwenda, kulikuwa na dunia mpya na furaha na akasema “Ingia kwenye furaha ya Bwana ambayo uli….



Uliyowekewa tangu kuwekwa misingi ya dunia”. Unaona?

Na oh nikawaza. “Wanaingia pale na wanasalimiana na wanafurahia na wanaenda juu ya milima na sehemu kuu” Nikawaza, oh! Si hilo nila ajabu. Utukufu haleluya. Kuruka tu juu na chini.

Halafu ningesikia jina lingine likiitwa, ningesema ninamjua huyo ninamjua huyo. Yule pale anaenda. Muangalie akienda juu “Ingia katika furaha ya Bwana, oh! Jamani zuri hilo na oh!” Nikasema “Mungu asifiwe, Mungu asifiwe”

Hebu fikiria, kama tu walikuwa wanasema Orman Neville unaona? Na halafu, ningesema, huyo ni ndugu Neville, huyo hapo, naye anatoka kutoka kwenye kundi anaenda juu kule, Namsikia Yeye akisema “Ingia kwenye furaha ya Bwana ambayo iliandaliwa kwa ajili yako kabla ya misingi ya dunia”. “Ingia” (Matayo 25:21). Na ndugu Neville angebadilika na angeanza tu kupiga kelele na kufurahi. Mimi nilikuwa tu na piga kelele na kusema “Utukufu kwa Mungu” mimi mwenyewe nimesimama hapa nikiwa na wakati mzuri sana. Nikiangalia ndugu zangu wakiingia ndani.

Na Malaika anayerekodi alisimama na kusema “William Branham”

Kamwe sijafikiri kwamba ningetembea hapo. Kwa hiyo niliogopa. Nikawaza oh mimi, nitaweza kufanya hivyo? Kwa hiyo nilienda nikitembea kuelekea hapo na kila mmoja tu akinipiga piga mgongoni kama hivi, juu, ndugu Branham (“Hi Bro Branham). Mungu akubariki wewe ndugu Branham” wakinipigapiga kadri nilivyokuwa ninapita kundi kubwa la watu Mungu akubariki, wewe ndugu”

Nilikuwa ninaenda nikisema, “asanteni, asanteni, asanteni” kama vile ninatokea kwenye mkutano au kitu fulani. Unajua na nilikuwa ninaenda kutembea sehemu hii kuu ya pembe iliyo kama ngazi.

Nikaanza kutembea juu pale na nikapiga hatua moja. Nikasimama, na nikafikiri…… Nikaangalia uso Wake, nikafikiri, “Napenda nimuangalie vizuri Yeye kwa upande huo” na nikasimama nilikuwa nimeweka mikono yangu hivi; Nikasikia kitu fulani kikiingia mkononi mwangu hapa. Ilikuwa ni mkono wa mtu mwingine. Nikaangalia kuzunguka, na yuko pale Hope, yale macho makubwa meusi na zile nywele za Brauni zikining’inia mgongoni, akiwa na vazi jeupe akiniangalia kama hivi.

Nikasema “Hope”. Nikasikia kitu fulani kikipiga mkono huu, unajua, kama hivyo. Nikawa nao mikononi mwangu na hapa tunaenda nyumbani.

Oh! Nikaamka na nikuinuka na kukaa kwenye kiti na kulia. Unajua, niliwaza, “oh Mungu natumaini hilo linakuja kama hivyo” wote wawili tukiwa tumeshirikiana katika maisha kuleta watoto na mambo kama hayo, na tuko hapa tunatembea kuingia katika dunia mpya, oh mimi, ambapo ukamilifu na kila kitu. Hapana kitu…. Kwa nini itaenda kuwa kitu cha ajabu

sana. Usikose hilo; kwa neema ya Mungu fanya kila uwezavyo kufanya, na hapo itakuwa juu ya Mungu kuangalia yaliyobakia. [1]

Na ninajua sikumoja lazima nisimame kwenye kiti cha hukumu cha Kristo ili kutoa maelezo kwa yale tuliyoyafanya katika maisha haya. [2]

Sasa, kunaweza kukawa na mambo mengi ambayo siyajui, lakini ninamjua Yesu Kristo. Nafanya kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu. Na siku moja nitakutana na kila mmoja wenu katika kiti cha enzi cha Kristo, nitasimama pale, hiyo ni kweli. Nitatoa hesabu ya yale ninenayo na yale nitendayo. [3]

Kuna watu hapa ambao sitawaona kamwe mpaka nitakapo waona kwenye kiti cha hukumu cha Kristo. [4]

Na ninashukurani--- wengi wenu ninyi watu ni maskini na usiku wa leo na pengine utaweka senti yako ya mwisho uliyo nayo. Na katika siku ile kuu, tutakaposimama pale katika kiti cha hukumu cha Kristo, na unasikia wale wapagani wakilia, wakati baada ya kusikia jina langu likiitwa, na inabidi ni inuke na kusimama katika ule mkanda unasao nao utachezwa na tazama kile kioo kitaonyesha vyote, na watu hawa wenyeji na makafiri kutoka nchi mbali mbali, wakisema "oh ndagu Branham, kama kama usingeenda, ningepotea na Mungu atakuangalia wewe na kusema "Ilikuwa ninyi ndio mlimtunza"

Kama kuna baraka ipaswayo kutokana na hiyo uipokee, kwa sababu siifanyi hivyo kama kazi. Kila mmoja wenu angeweza kuifanya. Mungu alinituma mimi, na ni ninyi mnanisaidia mimi kwenda. Mungu na awabariki sana na awarudishie mara mia. [5]

Kama sitawaona ninyi tena; nitakapokutana nanyi pale katika kiti cha hukumu cha Kristo ambacho wote tutakutana, kumbuka nimewaambia ilivyo kweli [6] Na ninapaswa kuwajibika kwa kile ni --- Mungu atanifanya ni wajibike [7]

Kama nitarudi tena mwaka ujao, kuna wengine wetu hawatakuwa hapa. Mnajua hilo. Huu utakuwa ni mkutano wetu wa mwisho hapa duniani. Halafu tutakutana mmoja kwa mwingine tena. Hapo itakuwa kwenye kiti cha hukumu, au kiti cha hukumu cha Kristo. Utasimama pale ukiwa aliye hesabiwa haki au asiye hesabiwa haki. Itakuwa umechelewa hapo. Huwezi ukafanya chochote juu ya hilo. Na unajua na unaamini, kwamba Mungu kupitia Biblia Yake hapa amethibitisha tena na tena uwepo wake upo hapa (1korintho 3:11-15). [8]

"Itakuwa lini, ndugu Branham"? siwezi kukuambia. Lakini moja ya hizi siku, kama tutakutana tena hapa duniani, tutaenda kukutana ng'ambo kule kwenye kiti cha hukumu cha Kristo.

Ninamshukuru Mungu kwa Neno lake; Namshukuru Yeye kwa ajili ya Yesu Kristo. Kwa maana bila Yeye kumtuma kwa ajili ya upatanisho wa dhambi zetu; Sote tungekuwa kwenye matope mengi ya dhambi bila ya



matumaini. Lakini kwa Neema Yake, Damu Yake hutuosha na dhambi zote. (1 Yohana 1:7-9; Ufunuo 1:5-6). Kama tu tone la wino katika ndoo ya Blichi, hutaliona tena kamwe. Dhambi zako zinapotubiwa, zinawekwa katika Damu ya Yesu Kristo; hazitajulikana tena kamwe (Warumi 8:1-2). Mungu anazisahau tena hizo; zilikuwa kamwe hazikufanywa. Na ili mradi ile sadaka iko pale, basi kuna upatanisho kwa dhambi zetu, iko hivyo…… unaona? Sisi sio wenye dhambi tena; sisi ni wakristo kwa Neeme ya Mungu [9]

Na alikuwepo kijana mdogo pale; nafikiri ni hawa mastaa watu wacheza sinema. Jina lake ni Danny Henry, naye alikuwa ni kijana mbaptisti. Vema alikuja hapa madhabahuni ili kunikumbatia mikononi mwake, na akasema, ndugu Branham, naamini ni hii siyo isikikayo kama mzaha "Lakini akasema naamini hiyo inaweza ikawa kama sura ya 23 ya Ufunuo"

Na mimi nikasema. "Asante"

Na akaanza kusema jambo lingine tena na akaanza kunena kwa lugha, kijana wa kibaptisti. Na alipofanya hivyo, alikuwepo mwanamke aliyetokea hapa lousiana; alikuwa ni mfaransa alikuwa mwanamke mnene; akaandika ile tafsiri.

Vema, alikuwepo kijana mdogo aliyekuwa ameketi hapa alikuwa ni mfaransa; aliandika kile alichosema. Walilinganisha walichoandika, na zote mbili zilikuwa sawa kabisa.

Na halafu kijana mkubwa, aliyekuwa amesimama kule mbali nyuma alitembea kuja huku akasema naomba nione hayo waliyo andika. [10]

Sasa huu hapa ujumbe wenyewe: kwa sababu umechagua njia nyembamba, njia iliyo ngumu; umetembea katika chaguo lako mwenyewe; umechagua na kuchukuwa uamuzi ulio sahihi na hiyo ndiyo njia yangu. Kwa sababu ya uwamuzi huu, sehemu kubwa ya Mbingu inakungojea wewe. Umefanya uwamuzi wa utukufu. Kwa huu wenyewe ndio utakaoleta na kufanya uje ule ushindi wao mkuu katika upendo wa kiungu. [11]

Jinsi itakavyokuwa jambo la kutisha kwa wale ambao wakati tarumbeta ya mwisho itapigwa, na vita vya mwisho vimepigwa, na mahubiri ya mwisho yamehubiriwa, na wakati wimbo wa mwisho utakapoimbwa na tunasimama kwenye kiti cha enzi cha Kristo. Na utaenda kuulizwa "kwa nini ulishindwa kulipokea hilo? Ulifanya nini na uhai niliokupa?" Utaulizwa na utatakiwa kutoa sababu. Itakuwaje? (Warumi 14:10-12). [12]

Na ndugu zangu, hebu niseme hili kwa kicho na heshima kwenu ninyi ndugu zangu, nikijua kuwa pengine kabla ya usiku huu tutakuwa tumesimama penye kiti cha enzi cha Kristo kule mbinguni…….. [13]

Na kumbuka hili: ninapaswa kusimama mbele za kila mmoja wenu katika kiti cha hukumu cha Kristo. Nitakutana na ninyi pale, na nitawajibika kwenu. [14]

Tunaweza kuomba. Baba wa Mbinguni, ambaye tunampenda na kumtegemea, tukijua hili….. kama mhuduma, kuhani, ni kihudumu vitu vya kiroho kwa watu, nikisimama usiku wa leo hapa kati ya walio hai na walio kufa, nikijua hili, kwamba siku moja bila kivuli cha shaka, itabidi nijibu kwa kila Neno mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Kuona wanaume na wanawake hapa, watu wapendwa, wanafanya chochote ningewaambia wafanye, Baba. [15]

Nilikuwa na ono sio muda mrefu uliopita, na nikaangalia pale, na nikawaona watu hawa wote pale, walikuwa mamilioni yao. Na nikasema, "Una maanisha anakuja kwangu" Wakasema "Ndio, na halafu tumerudi duniani pamoja nawe" nikasema, "Je kila mhuduma atapaswa kusimama hivyo?"

Ndio, Bwana, kila mhudumu atasimama katika huduma yake na kusanyiko lake? Akasema, "Ndiyo, Bwana" (Huyu malaika aliyekuwa akizungumza nami alisema hivyo.)

Na nikasema, basi hata Paulo itabidi asimame pia?

"Paulo atasimama na watu wa kizazi chake.

Nikasema; "Hapo najua niko sawa tu kwa sababu nilihubiri Neno kwa Neno sawa na alivyofanya". Na nilipofanya hivyo, mamilioni wakalia kwa sauti, "Hapo ndipo tunapo simamia" Amen katika hilo Neno, hilo Neno, haijalishi ni nini, lile Neno (Warumi 14:10-13). [16].

Na wakati nikiwa nimelala pale nikasikia kitu Fulani kikisema kwa wazi kama unavyosikia sauti yangu Endelea kupambana tu (keep pressing on). / endelea kukandamiza tu. Inakuja kwa njia ambayo ni kama hayo maono hapa. Unalisema na hujui kama umelisema hilo. Unazungumza unanena, hujui una nena. Ninapoona ono mbele ya mtu sijui kile nilichosema. Ni vile tu nijuavyo hilo naenda nyuma kwenye kanda na kulitafuta. Sijui nilichosema kwa sababu uko mahali pengine sehemu nyingine, pengine miaka arobaini au hamsini nyuma katika maisha ya mtu au mbele kule katika maisha ya mtu, hujui; hujui hilo ambalo unalisema. Na nikasema ninakazana/ninakandamiza tu. Akasema Endelea kukazana tu; "Endelea kukazana tu" ikasema, "Thawabu/ tuzo kuu ni mwisho wa safari"

Nukuu za kiingereza.

[1] Muhuri wa sita kitabu cha mihuri uk 453-470
[2] Ni nani aliye sadiki Ripot yetu? (51-0719)Aya. E-20
[3] Imani waliyokabidhiwa watakatifu (53-1129A).Aya E-129
[4] Yesu Kristo ni yule yule (52-1027) Aya E25
[5] Uponyaji wa kiungu 54-0620E Aya E-14
[6] Ushawishi(64-0315,Aya E-9
[7] Nenda kamuamshe Yesu (63-1103),Aya E-110
[8] Ni mimi, Msiogope (62-0726),Aya E-83



[9] "Ule muhuri wa saba" Kitabu cha mihuri ul.568

[10] Kujaribu kumfanyia Mungu kazi (65-1127B ),Aya 32
[11 Utungu wa uzazi (65-0124),uk.2
[12] Ufunuo sura ya 4 sehemu ya 1 (60-1231),Aya 111
[13] Ripoti ya safari ya India (57-0126B)Aya E-26
[14] Kujitenga na kutokuamini (55-0228)Aya E-57
[15] Mwaka wa jubilee (54-1003E)Aya 155
[16] Kukataliwa kwa uwakilishi (60-1113) Uk. 32
[17] Kutoka ule wakati (60-0716)Aya E-88.

*jiwe la kiroho la kujengea na 180 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*